

Toweni Mauwa Kwa Walio Hai
(Give Flowers To The Living)

Na

John Kombo

Toweni Mauwa Kwa Walio Hai

(Give Flowers To The Living)

Na

John Kombo

Desemba 22, 2014

Toweni Mauwa Kwa Walio Hai

Wakati wa msiba wa mpendwa au rafiki tumezoea kuweka mauwa ikizunguka jeneza na kufunika kaburi kwa mauwa baada ya kuzika. Yote hii ni vyema na nzuri na hushukurwa na wanafamilia, lakini aliyefariki hajui lolote kulihusu. Ingekuwa bora kiasi gani kama tungewapa walio hai mauwa hayo.

Nilimpoteza mama yangu; Bi. Jeskah Nandwa akiwa na umri wa miaka 90. Nilisimama pembeni ya jeneza ambalo lilikuwa na mwili wake uliyokuwa hauna uhai tena na kutazama macho yake yaliyofumbwa; yasingeweza kuona. Mikono yake ya baridi isingeweza kushika kitu. Pumzi iliyositishwa isingeweza kukusanya upepo mwanana kutoka katika mauwa ambayo yalikuwa katika mikono ya ndugu. Nilikuwa nafikiria ni kiasi gani nimempa mama yangu alipokuwa hai.

Kila siku tunayoishi, tuna nafasi ya kuwekaa mauwa kwa mtu aliye na hitaji. Mtu Paulo anatuambia katika Gal. 6:10, "...*kila tupatapo nafasi na tutende mema kwa kila mtu, hasa nyumbani mwa waaminio.*" Maneno haya ya Paulo yanafunika sehemu kubwa ya huduma ambayo tunaaweza kutoa. Mara zote kuna ndugu au jirani anayeitaaji kutiwa moyo. Na kutoa faraja kwa mtu aliyekata tamaa ni zaidi ya wajibu wa Mkristo kama kumrekebisha anaye enenda bila utaratibu (1 Thes. 5:14-15).

Kwa nini tunasubiri hadi mtu afariki ndipo tunaonyesha hisia zet, "Tuwape mauwa yetu wangali hai." Hii inahusiana na wale wote waliofanya chochote katika maisha yetu – kama tuna bahati ya baba na mama wakiwa hai, wazee katika kanisa, waalimu wa zamani na wahubiri, na marafiki waliotusaidia kuwa na ujasiri na kufanya uchaguzi mzuri katika maisha. Tusimame na tufikiri; kila mmoja wetu anawiwa zaidi, tafadhali usisubiri hadi wafe; onyesha shukrani zako wakiwa hai! Biblia inasema, "*Enyi watoto watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi, upate heri ukae siku nyingi katika dunia.*" (Efe. 6:1-3). Kama kuna chochote kinachoweza kufanya "damu ya mtu ichemke," ni kuwasikia watoto wakiongea kwa dharau kwa wazazi wao, hasa mama zao, ambao zaidi waliteseka nusu kufa kwa kuwaleta hapa duniani.

Siku moja, ninyi vijana, mtasimama pembeni ya jeneza na kukumbuka muda umeenda na kusema, "Samahani" wazazi wakiwa wamezeeka na kushindwa kujihudumia pamoja na watoto, ambao wamejitoa zaidi katika kuwalea, kusimama kwa kidogo au kisiwepo, siku moja wataikumbuka, labda milele. Zaidi ya miaka, nilipokuwa na nafasi ya kuhudhuria mazishi ya wazazi wenye umri mkubwa,

nimekuwa nikiona hilo, kama sheria, anayeichukua ndiyo yule anayekuwa makini katika maisha.

Waume na wake, wakati utafika ambapo mmoja wenu atasimama katika mfumo wa maisha ambao haupo ya mwingine na kunena maneno mazuri na yenye upendo ambayo masikio yao hayata sikia. Sasa ndiyo wakati ulio na nafasi ya kunena maneno hayo mazuri! Kwa nini usubiri hadi wafe? Wana njaa sasa ya kukusikia ukisema, “Ni nana kupenda!” wanaume, ni muda gani umepita toka umwambie mkeo kuwa ni mzuri? Paulo alisema, “*Enyi waume wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake,*” (Efe. 5:25).

Tena, “*Ninyi waume wapendeni wake zenu msiwe na uchungu nao.*” (Kol. 3:19). Wake, ukarimu wenu utawafanya waume zenu wawape usikivu mnaostahili.

Kuna zaidi na zaidi, lakini haya ni machache katika nafasi nyingi ambayo huja kwetu kutoa mauwa kwa walio hai. Ni maombi yangu kwamba yaweze kutumika na kutukumbusha umuhimu wa kufanya nafasi bora ijayo kwetu kila siku ili kwamba hakika “tuukomboe wakati” na kutumia kila siku kikamilifu kadiri iwezekanavyo kwa utukufu wa Mungu.

John Kombo

Nakuru, Kenya

